



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA LUDEWA**



Oktoha 29, 2022

BARAZA LA MADIWANI LA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2022/2023

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Mhe. Wise Mgina ameongoza mkutano wa baraza la Waheshimiwa Madiwani Wilayani Ludewa uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri leo Oktoba 29, 2022.

Mkutano huo ni wa robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023 wa kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2022 wa tarehe 29 Oktoba, 2022.

Viongozi mbalimbali wamehudhuria wakiwemo viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Mwakilishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ludewa, Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wilaya ya Ludewa wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Ndg. Sunday Deogratias na wananchi wa Wilaya ya Ludewa.

Pamoja na mambo mengine Kamati ya kudhibiti UKIMWI (CMAC), Kamati ya huduma za Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Kamati ya Elimu, Afya na Maji pamoja na Kamati ya Fedha na, Uongozi na Mipango zimewasilisha taarifa za utekelezaji kwa robo ya kwanza 2022/2023.

Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Wilaya ya Ludewa.